# TANGAZO LA ZABUNI

**ZABUNI YA UWAKALA WA USAFI WA MAZINGIRA NA UKUSANYAJI WA ADA YA UZOAJI TAKA NGUMU KATA YA BOMANI TAREHE 01 OCTOBER 2025.**

5. Ofisi ya mtendaji kata ya Bomani inakusudia kupata wazabuni wenye uwezo wa kufanya usafi wamazingira, kuzoa taka na kuzisafirisha kwenda dampo la Magena kutoka katika maeneo ya makazi, biashara, masoko, maeneo ya wazi na taasisi mbalimbali zilizopo kata ya Sabasaba na ukusanyaji wa ada ya usafi wa mazingira kila mwezi kutoka kwa wanufaika wa huduma ya uzoaji taka kwa kutumia POS mashine za Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia November 1, 2025 hadi June 30, 2026.
6. Kata ya Bomani inapenda kuwaalika/kuwatangazia wakandarasi, watu binafsi, makampuni, mashirika, Vikundi au Taasisi za umma zilizosajiliwa kisheria wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hizo kutuma maombi yao kwa zabuni kama ifuatavyo

**A: UWAKALA WA USAFISHAJI WA MAZINGIRA NA UKUSANYAJI WA ADA YA UZOAJI TAKA NGUMU** utajumuisha mitaa ifuatayo

- mitaa ya Mawasiliano, NHC, Anglican, Bomani, Magereza, Biambwi na Buhemba).

**MASHARTI YA JUMLA.**

33. Nakala ya leseni hai (isipokuwa CBOs) hazihusiki na sharti hili
34. Waombaji wote waambatanishe nakala za usajili wa makampuni yao au vikundi vya kijamii (CBOs) au Taasisi.
35. Vikundi vya kijamii (CBOs) viambatanishe orodha ya viongozi wa kikundi na barua za utambulisho kutoka kata husika.
36. Waombaji wote waambatanishe nakala za VAT au TIN
37. Mwombaji ni lazima aambatishe wasifu wa kampuni (company profile) au kikundi CBO's profile au Taasisi
38. Waombaji wawe na visibitisho vya kuwa na vitendea kazi kama vile magari/trekta kwa ajili ya kusafirisha taka kwenda dampo, vifaa vya kutosha kusafishia, wafanyakazi/vibarua wa kutosha kutokana na ukubwa wa eneo pamoja na ofisi ya kudumu. Au aeleze kwa kuambatanisha uthibitisho kuwa amekubaliwa kukodi magari.
39. Ili kuhakikisha afya na usalama kwa wafanyakazi watatakiwa kupima afya zao mara mbili kwa mwaka na pia wawe na vifaa kingaa kama vile ovaerall, vizuia harufu mbaya, safety boot na heavy duty gloves.
40. Mwombaji/waombaji anatakiwa kuambatisha picha za mkurugenzi /wakurugenzi/meneja/mwenyekiti/katibu wa kampuni yao katika maombi yake

CamScanner

41. Kamati ya tathimini itakagua ofisi, magari ya kusafirishia taka, vifaa vya usafi, vielelezo mbalimbali vilivyo tajwa hapo juu vya mwombaji na kutoa mapendekezo kwa kitengo cha manunuzi.
42. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na kata. Aidha, mwombaji aliyewahi kushitakiana na kata kuhusianana kazi yoyote hatopewa nafasi ya ushindani kwa kazi yoyote ya zabuni iliyotangazwa na kata. Vilevile waombaji wote watakaothibitika kuwa na tuhuma za utendaji usiozingatia sheria kutoka taasisi nyingine za serikali hawatopewa nafasi ya ushindani kwa kazi zitakazotangazwa.
43. Mwombaji yeyote atakayeshndwa kutimiza au kutokamilisha maelekezo ya masharti hayo ya zabuni atakuwa amejiondoa mwenyewe katika ushindani.
44. Mzabuni atakayeshinda zabuni atatakiwa kuweka dhamana (bond) ya makisio ya makusanyo ya miezi mitatu (3). Dhamana hiyo itarudishwa baada ya mkataba kuisha na endapo mzabuni atashindwa kutimiza masharti ya mkataba dhamana hiyo itatumika kutekeleza shughuli za sehemu ya mkataba mpaka atakapopatikana mzabuni mpya.
45. Zabuni zote zifungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri (seal), na juu ya bahashaa iandikwe maandishi yanayotaja zabuni na ipelekwe katika ofisi ya mtendaji wa kata. Juu ya bahasha iandikwe zabuni anayoomba, maombi yote yatumwe kwa MTENDAJI WA KATA YA BOMANI, S.L.P 45, TARIME.
46. Tarehe ya mwisho wa kupokea maombi ni siku ya jumatatu Oct 7, 2025 saa 9.30 Alasiri na ndiyo siku ya ufunguzi wa zabuni hizi. Waombaji au wawakilishi wao watakaopenda kuhudhuria ufunguzi wanaruhusiwa kuhudhuria.
47. Maombi yatakayofika baada ya muda uliowekwa kuisha hayatapokelewa na hayatafunguliwa.
48. Mzabuni atakaeshinda tenda atasaini mkataba wa kazi na mkataba huo utasainiwa mbele ya mwanasheria wa Halmashauri ya mji wa Tarime.

Rosemary Karoli
AFISA MTENDAJI KATA
BOMANI

AFISA MTENDAJI
KATA YA BOMANI
TARIME